# 8. MTAALA MPYA NA UTENDAJI WA WANAFUNZI WA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA UPILI MJINI MBARARA

- **Murokozi Cranimah**
- **Bishop Stuart University, Department of Languages**

## IKISIRI

Utafiti ulikuwa unahusu kutambua mchango wa mtaala mpya katika ufundishaji wa wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili zilizochaguliwa jijini kusini mwa Mbarara na ulilenga kutambua umuhimu wa mtaala mpya katika ufundishaji wa wanafunzi wa Kiswahili katika shule za upili, kuchunguza changamoto zinazokumba wanafunzi na walimu wa Kiswahili katika ufundishaji wa mtaala mpya na kutambua njia zinazotumiwa kutatua changamoto zinazosababishwa na mtaala mpya. Watafiti walituia mbinu ya maelezo, Watafiti walikuwa makini katika kueleza, kufafanua, kuhakiki, kuvumbua, kufanya majaribio, kutafsiri taarifa walizozipata kupitia muundo huu wa utafiti. Sehemu ndogo ya utafiti ilitumia takwimu kama kielelezo na ulifanyika katika shule za upili zilizochaguliwa jijini kusini mwa Mbarara, Utafiti huu ulilenga walimu na wanafunzi wa shule za upili wanoajifunza lugha ya Kiswahili. Katika utafiti huu taarifa mbalimbali zilikusanywa kutoka maktabani na uwandani kwa kutumia mbinu na vifaa mbalimbali vilivyoandaliwa na watafiti. Watafiti walichunguza na kuchanganua data za watafitiwa kulingana na kiwango cha jinsia na umri katika shule za upili.

Utafiti huu ulihitimisha kwamba mtaala mpya wa Kiswahili unahusiana sana na utendaji kitaaluma kwa wanafunzi wa fasihi ya

Kiswahili lakini ili kuiendeleza mtaala mpya ipasavyo ni jukumu la walimu wakuu, walimu, wazazi, wanafunzi, serikali pamoja na kituo kikuu cha mtalaa ni lazima kujiunga pamoja kwa lengo moja na ulipendekeza kwamba Wizara ya elimu iangalie kwamba walimu wamepewa elimu ya ziada kuhusu mabadiliko ya mtaala mpya ili kupata ujuzi na stadi za kufundisha vyema. Walimu wakipewa elimu ya ziada wanapata stadi na hamu ya kwendeleza mtaala mpya jambo linaloletea wanafunzi kufaulu mitihani kwa sababu watakuwa wanapata mwongozo mzuri kutoka walimu, Pengine lazima viongozi wa shule wajaribu huku na kule kuona kwamba wamenunua vitabu vya kiada na vifaa vingine kama miongozo ya walimu inayofasili vitabu vya kiada. Jambo hili huwezesha walimu kufundisha bora wanafunzi na mwishoni wanazuka na utendaji bora kitaaluma.

**ABSTRACT**

[English Translation]

This research was about the impact of the new curriculum on the performance of Kiswahili students in secondary schools in Mbarara town. This study aimed to explain how the new curriculum is implemented in schools, identify the challenges faced by Kiswahili students and teachers in the teaching of the new curriculum and clarify the ways used to address the challenges posed by the new curriculum. In this study, the researcher will be inspired by the theory of learning discovery. This theory was developed by Bruner (1966). According to Bruner, the theory of cognitive learning holds that it is good for students to learn by relating what is being taught to the context of reality. The use of materials in teaching and learning can bring realism and thus guide students to innovate on their own and make grammar easier faster. This research will be conducted because it is believed that when

the new curriculum is used in an efficient manner, it can improve the teaching and learning of Kiswahili in secondary schools. The research approach in this work will be descriptive. The researcher will be carefully explaining, explaining, reviewing, innovating, conducting experiments, interpreting the information he will obtain through this study design. The researcher went to the field to conduct interviews with the respondents as well as disseminating the arguments. In total the researcher had 90 respondents. This figure was achieved by appointing 4 Kiswahili teachers and 26 Kiswahili students from each school so a total of 90 researchers will be selected from three schools. This research required 90 respondents. Research of this kind strongly emphasizes the use of accurate measurements and data analysis using data available in the field through interviews, and arguments. This kind of research can also be done by analyzing existing data statistics without going to the field. However, according to this study, the researcher will go to the field to collect data that he analysed.

This research concluded that the new Kiswahili curriculum is closely related to the academic performance of Kiswahili literature students. However, to effectively implement the new curriculum, it is the responsibility of headteachers, teachers, parents, students, the government, and the central curriculum authority to come together with a common goal. It suggested that the Ministry of Education should ensure that teachers receive additional education regarding the changes in the new curriculum to acquire the skills and abilities to teach effectively. When teachers receive extra education, they gain skills and enthusiasm for advancing the new curriculum, which results in improved exam performance for students because they receive proper guidance from their teachers. Perhaps school leaders should make efforts to ensure they have purchased textbooks and other materials, such as teacher guides that explain the textbooks.

## UTANGULIZI

Utafiti huu utafanywa ili kutathmini athari za mtaala mpya katika utendaji wa wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili zitakazochaguliwa mjini Mbarara. Sura hii inazingatia Usuli wa utafiti, Tatizo la utafiti, Malengo ya utafiti, Maswali ya utafiti, Upeo wa utafiti na Umuhimu wa utafiti.

Mtaala ni dhana pana ambayo haina maelezo ya aina moja. Katika kufasili dhana hii, wataalamu mbalimbali wamekuwa wakitofautiana kutokana na kuwa na mitazamo tofauti. Kwa ufupi ni kwamba dhana ya mtaala, inajumuisha nadharia na modeli ambapo hili ni eneo la taaluma lenye mitazamo tofauti (TET, 2013). Mtaala huonesha maudhui, vyanzo vya maarifa, stadi na tabia anazotarajiwa kuwa nazo mlengwa, lakini pia, mtaala unaonesha njia muafaka za kufanya tathmini, ufuatiliaji na utahini.

Mtaala wa Dunia unaendelea kubadilika ili kuendana na mahitaji ya sasa. Mabadiliko hayawezi kuepukika kwa wote nchini, bila kujali hali ya kisiasa, kijamii au kiuchumi. Aytac na Deniz, (2010). Wanafunzi wanatarajiwa kuwajibika kwa wao wenyewe kwa kujifunza kupitia uchunguzi wa moja kwa moja na uzoefu wakati walimu wao wanatarajiwa kubuni mafunzo yenye ufanisi kwa kuwapa shughuli zinazolenga maendeleo ya uwezo maalum. Aidha, mtaala mpya uliorekebishwa unahitaji walimu kutathmini wanafunzi wao mara kwa mara kwa kutumia mbinu za tathmini, kama vile miradi ya uchunguzi wa darasani na uwanja, mawasilisho ya mdomo, tathmini binafsi, mahojiano na tathmini za rika. Walimu pia wanahitajika kubadili ufundishaji wao kutoka kwa mbinu za kawaida zinazorejelewa hadi kigezo-hukumu iliyorejelewa ya uwezo wa wanafunzi au uwezo wa kuamua maendeleo yao. Hatimaye, walimu wanatakiwa kutoa maendeleo endelevu, kwa wakati na maoni yenye kujenga ili kuwafahamisha wanafunzi kuhusu nguvu na udhaifu ya utendaji wao. (Bhattacharya, 2021).

Hapo nyuma mtaala ulionekana kama mwongozo wa kufundishia (muhtasari wa somo), au mpangilio wa programu ya ufundishaji. Kwa mujibu wa TET (2013) hivi sasa, mtaala ni mwongozo mpana unaoweka viwango vya utoaji elimu kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo: (1) Ujuzi watakaoujenga wanafunzi yaani maarifa, stadi na mwelekeo; (2) Njia za kufundishia na kujifunzia zitakazotumika katika utekelezaji wa mtaala; (3) Vifaa vya kufundishia na kujifunzia

vinavyohitajika; (4) Upimaji, ufuatiliaji na tathmini ya mtaala unaohusika; (5) Sifa za kitaaluma na kitaalamu za mwalimu atakayeufundisha mtaala unaohusika; (6) Miundombinu wezeshi kwa ajili ya utekelezaji wa mtaala wenye ufanisi; na (7) Muda utakaotumika katika ufundishaji au utekelezaji mtaala. Vipengele hivyo, ndio huunda mtaala wa ufundishaji wa somo linalohusika katika ngazi fulani ya mafunzo.

Neno mtalaa vilevile linamaanisha matarajio, malengo, na maudhui ambayo mwanafunzi anatarajiwa kuyakamilisha kabla ya kutunukiwa tuzo ya kitaaluma katika ngazi Fulani. kuna aina mbalimbali za mtalaa. Kuna mitaala ambayo imeandikwa na ambayo haijaandikwa, kuna mitalaa inayoonekana na isiyoonekana. Kimsingi mtalaa ni mambo yote ambayo mwanafunzi hupitia katika kujifunza tangu anapojiunga na mfumo rasmi wa elimu hadi anapohitimu katika ngazi Fulani ya elimu ikiwemo malengo ya elimu, maudhui, njia na nyenzo za kujifunza na njia za tathmini.

Mitaala ya Ufundishaji Kiswahili Sekondari hapa Uganda imegawanyika katika sehemu kuu tatu kulingana na ngazi inayohusika. Sehemu ya kwanza ni Mtaala ya Kiswahili Sekondari ngazi ya kwanza (Kidato cha I-II), sehemu ya pili ni Mtaala wa Kiswahili Sekondari ngazi ya pili (Kidato cha III-IV), na sehemu ya tatu ni Mtaala wa Kiswahili Sekondari ngazi ya tatu (Kidato cha V-VI). Katika makala haya tunatathmini Mtaala wa Kiswahili Sekondari ya kiwango (Kidato cha I-II). Mitaala iliyopo hivi sasa imetolewa kwa kuzingatia ngazi ya elimu. Mitaala ya Kiswahili sekondari inayotumika ilitolewa mwaka 2021.

Aidha, kama ilivyodokezwa katika ufafanuzi wa dhana ya mtaala kwamba mojawapo ya kipengele cha mtaala ni maudhui. Hii hujumuisha ujuzi, malengo na mada zitakazofundishwa. Mwongozo unaofafanua kiwango cha maudhui kwa mwanafunzi kwa kuzingatia umri, ujuzi, malengo na mada kwa kila darasa huitwa muhtasari (TET, 2013). Hivyo basi, kuna uhusiano wa karibu sana kati ya mtaala na muhtasari kiasi kwamba watu wengine inawawia vigumu kutofautisha dhana hizi. Hata hivyo, itaonekana wazi kuwa wakati mtaala ni mwongozo wa uendeshaji wa shule, muhtasari unalenga kutoa

maelekezo ya namna ufundishaji na ujifunzaji utakavyotekelezwa ndani ya darasa. Hivyo, maelekezo hayo yanajikita katika kila somo linalofundishwa.

## SUALA LA UTAFITI

Kothari (2014) anaeleza kuwa Tatizo la utafiti linarejelea ule ugumu anaouona mtafiti ama katika nadharia au vitendo na hivyo anataka kupata ufumbuzi wa tatizo hilo. Anachoeleza Kothari ni kwamba tatizo la utafiti linatokana na uwepo wa tatizo linalohitaji kutafutiwa ufumbuzi au suluhisho. Kumekuwa na tafiti kadhaa ambazo zimeonesha kuwa wanafunzi wengi hawafaulu vizuri katika stadi ya sarufi (Njogu 2015). Kutokana na dai hili, mtafiti aliamua kuchunguza mtaala mpya wa sekondari nchini Uganda katika somo la Kiswahili kama unavyochangia katika utendaji bora wa mwanafunzi.

Kutokana na mabadiliko katika silabasi ya Kiswahili (NCDC 2020). Mbinu za kufundisha lugha ya Kiswahili zimebadilika kwa kiasi kikubwa pamoja na utaratibu wa mada hasa kutoka kidato cha kwanza kwenda kidato cha pili kwa mfano, katika mtalaa uliopita waalimu waliongozwa na vitabu kama vile vya Milton Rwabushaija kufundisha sarufi na misamiati bila kuingiza mada kama insha , ufahamu na mada nyingine ambazo zilifundishwa katika kidato cha tatu na kuendelea. Ufundishaji vilevile unapaswa ujikite sana kwa upande wa mwanafunzi kwa kugunduwa mambo tofauti kivyake pamoja na kujadiliana katika makundi tofauti na hali ilivyokuwa katika malaa uliotangulia. Ni katika misingi hii ndipo utafiti huu uliwania kuchunguza jinsi mtaala mpya unavyochangia katika utendaji wa wanafunzi wa Kiswahili katika shule za upili.

## UMUHIMU WA UTAFITI

Utafiti huu utasaidia walimu na wanafunzi na hata wazazi kwa kuwajulisha umuhimu wa mtaala mpya katika ufundishaji wa wanafunzi.

Utafiti utasaidia katika kutambua changamoto zanazosababishwa na mtaala mpya na hata kitasaidia katika kutambua suluhisho au njia za kutatua changamoto hizo.

Wanafunzi wataweza kutenda bora kitaaluma baada ya kufundishwa na walimu wakitumia vitabu ambavyo vipo kwenye silabasi kwasababu walimu watapata kujua silabasi mpya kutokana na utafiti huu. Pia utafiti huu utasaidia walimu wa Kiswahili kuelewa jinsi ya kutumia vitabu vya mtaala mpya Kwa ajiri ya kufundisha wanafunzi wa kiswahili wa shule za upili.

Utafiti utawasaidiatafiti kwa kukuza stadi ya utafiti. Pia watafiti atasaidiwa kufuzu katika kupata uzamili katika elimu kwa sababu utafiti ni moja wapo wa mahitaji ya chuo ili kuhitimu na uzamili.

## KIUNZI CHA NADHARIA

Kwa mujibu wa TUKI (2004) Kamusi ya Kiswahili Sanifu, nadharia ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua, au kutekeleza jambo fulani. Massamba (2004:64) anasema "Nadharia ni kanuni na misingi ambayo hujengwa katika msingi wa mawazo ili kutumiwa kama kiolezo cha kuelezea jambo".

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya ujifunzaji kiugunduzi yake Bruner (1966). Nadharia ya ujifunzaji kiugunduzi, hushikilia kuwa, ni vizuri kwa wanafunzi kujifunza kwa kuhusisha kile kinachofundishwa na mazingira ya hali halisi. Matumizi ya vifaa katika ufundishaji na ujifunzaji huweza kuleta uhalisia na hivyo kuwaongoza wanafunzi kuvumbua wenyewe na kurahisisha uelewekaji wa sarufi kwa haraka. Utafiti ulifanywa huku ikitiliwa maanani kuwa mtaala mpya ukitumiwa kwa njia inayofaa, huweza kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari.

Bruner (1966), alitilia mkazo nafasi ya mazingira na tajriba katika kukuza uwezo wa kiakili. Kwa kuwa alikuwa na shauku ya kuchunguza lugha na uwasilishaji wa mawazo ya binadamu, Bruner (1966), alichunguza maendeleo ya kiugunduzi katika lugha ya watoto. Kutokana na uchunguzi wake, Bruner (1966), alipendekeza kuwa, kwanza mwanafunzi anafaa kuwa mshiriki katika kila mchakato tendi ambao wanafunzi huibuana kubuni dhana mpya zilizo na msingi kwenye yale wayafanyayo. Anaendelea kusema kuwa, mwanafunzi huteua dhana alizojifunza na kuzigeuza au kuzitumia kupata maarifa mpya. Aidha Bruner (1990), anazidi kusisitiza kuwa, shughuli ya ufundishaji na ujifunzaji ni shughuli hai ambao huhitaji ushiriki wa mwanafunzi katika hatua zote za ujifunzaji.

Nadharia hii ina mihimili mitano ambayo ni:

Muundo bora wa ufundishaji na ujifunzaji. Katika mhimili huu, ufundishaji unafaa kuwa wa kidayolojia baina ya mwalimu na mwanafunzi. Mwanafunzi anafaa kuchukuliwa kama mhusika anayeshiriki kwa upana katika ufundishaji na ujifunzaji. Krashen (1988), anakubaliana na maoni haya ya Bruner (1966), anaposema kuwa, mbinu bora za ufundishaji ni zile zinazotilia maanani ushiriki mpana wa mwanafunzi anayeelekezwa na mwalimu. Kulingana na Krashen (1988), ufundishaji na ujifunzaji unaokuza uwezo wa ugunduzi ni matumizi ya vifaa katika ufundishaji na ujifunzaji.

Maandalizi kabla ya kuwasilisha somo ni muhimu katika kufanikisha ubora wa somo. Kwa mujibu wa nadharia ya kujifunza kwa ugunduzi, lengo kuu la ufundishaji na ujifunzaji ni kumpa mwanafunzi fursa ya kushiriki katika ufundishaji na ujifunzaji wala si kumwezesha tu mwanafunzi kupata dhana katika akili yake. Hill (1999), alihusisha nadharia hii ya kujifunza kwa ugunduzi na ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Anasema kuwa, mbinu bora ya kufundisha inayohusisha mwanafunzi katika hatua zote ni ile inayotumia vifaa vya kufundishia. Hill (1999), anashikilia kuwa, matumizi ya mtaala mpya humpa mwanafunzi fursa ya kuwa mshiriki mkuu katika shughuli nzima ya ufundishaji na ujifunzaji. Anawashauri

walimu kuhusisha matumizi ya vifaa halisi katika maandalizi ya masomo yao.

Mwanafunzi hupata maarifa zaidi kwa kutazama. Mhimili huu unashikilia kuwa, kwa ujumla, ujifunzaji ni matokeo ya mwanafunzi kuhusisha maarifa aliyoyapata kwa hali na miktadha mipya anayokumbana nayo maishani. Bruner (1966), anasema kuwa, ili mwanafunzi aweze kukumbuka dhana anazofundishwa, hana budi kupewa majukumuya kushiriki katika upataji wa dhana hizo. Anatilia mkazo nafasi ya mwalimu katika kubuni mazingira ambamo ujifunzaji hutokea na vile vile kumsaidia mwanafunzi kung'amua yale asiyoweza kufahamu kwa juhudi za kibinafsi.

Ari ya mwanafunzi ya kutaka kujua zaidi inafaa kuchochewa na mwalimu. Nadharia hii inaeleza kuwa, ili ujifunzaji upatikane, lazima kuwe na maingiliano kati ya funzo na mwanafunzi. Hapa matumizi ya mtaala mpya hufanikisha maingiliano hayo. Katika kiwango hiki, matumizi ya mtaala mpya humsaidiamwalimu kutoa mwelekeo zaidi ili kulifanya somo lake lieleweke kwa urahisi. Mwalimu anapaswa kuanza na mambo rahisi yanayofahamika kwa wanafunzi wote huku akielekea kwa mambo magumu. Katika mhimili huu, ufundishaji unafaa kuanza kwa kurejelea wanachokifahamu wanafunzi na kuelekea kwa kile wasichokifahamu.

Hapa wanafunzi huingia darasani wakiwa tayari na tajriba na maarifa fulani ambayo yanaweza kuwafanya kuelewa wanachofundishwa. Ufundishaji mzuri ni ule unaorejelea maarifa na tajriba hizo. Hill (1999), anahoji kuwa, matumizi ya mtaala mpya huwapa wanafunzi nafasi nzuri ya kutagusuna na tajriba hizi hivyo basi kuufanya ufundishaji na ujifunzaji kuwa rahisi.

Marzano (2011), akichangia kuhusu nadharia ya Bruner (1999), anasema kuwa, nadharia ya kujifunza kwa ugunduzi imebainisha kuwa ufundishaji ni mchakato ambao huhusisha kumtayarisha mwanafunzi kugundua mambo mwenyewe kwa kutazama au kusikia. Anaendelea kusema kuwa, kazi ya mwalimu ni kumwongoza mwanafunzi kwa kumpa maarifa yanayohitajika na

kumwacha mwanafunzi kugundua mwenyewe. Uongozi huu wa mwalimu kwa mwanafunzi huhitaji maagizo ya moja kwa moja.

Vile vile, Roya na Hanieh (2015), walichangia katika kuiboresha nadharia hii. Wanahoji kuwa, nadharia ya kujifunza kwa ugunduzi husisitiza jinsi wanafunzi wanafaa kuvitumia vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji kujifunza kwa njia bora zaidi. Wanazidi kuhoji kuwa, walimu wanafaa kutilia mkazo kile ambacho wanafunzi wanakifahamu na kuwapa fursa ya kuyaweka maarifa haya katika mazoezi. Kwa mujibu wa wataalamu hawa, ufundishaji na ujifunzaji unapaswa kuwa shughuli hai. Wanafunzi wanafaa kushirikishwa ipasavyo. Wanahoji kuwa, ufundishaji na ujifunzaji unafaa kuhusisha hali halisi. Hali hii itamwezesha mwanafunzi kuelewa dhana kwa njia bora zaidi.

Kwa mujibu wa Roya na Hanieh (2015), uhusishaji wa teknolojia ya kisasa kama simu, tarakilishi, runinga nakadhalika katika ufundishaji huwashirikishawanafunzi katika hatua zote za ujifunzaji. Hali hii huwapa wanafunzi motisha ya kufunza kwa njia bora zaidi. Wakimnukuu Hare (2005), Roya na Hanieh (2015), wanahoji kuwa maelekezo ya nadharia ya kujifunza kwa ugunduzi yanafaa kutiliwa maanani katika ufundishaji na ujifunzaji darasani. Hare (2005), anasisitiza kuwa, shughuli ya ufundishaji na ujifunzaji inafaa kuwashirikisha wanafunzi katika hatua zote. Kwa mujibu wa Hare (2005) uhusishaji wa teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji ni mbinu bora ya kuhakikisha kuwa wanafunzi wanashiriki ipasavyo katika somo. Akishadidia maelekezo ya Bruner (1966), Christie (2005), anahoji kuwa, mbinu bora ya ufundishaji na ujifunzaji ni ile ambayo inampa mwanafunzi fursa ya kugundua mambo mwenyewe.

Nadharia hii inasisitiza kuwa, wanafunzi wanafaa kushirikishwa katika ufundishaji na ujifunzaji. Bruner (1966), anaeleza kuwa, ufundishaji si kuhamisha maarifa tu kutoka kwa mwalimu hadi kwa mwanafunzi bali huhusisha jinsi mwanafunzi anashirikishwa katika mchakato huu. Bruner (1966), anazidi kuhoji kuwa, wanafunzi huingiliana na mazingira kwa kuchunguza na kutazama. Kwa hivyo, matumizi ya mtaala mpya huweza kuleta

athari hiyo ya kutazama na kuchunguza.

Kwa mujibu wa Bruner (1966), sifa kuu ya ufundishaji kwa ugunduzi, inahusu jinsi ambavyo watu hupata maarifa kutokana na matukio ya awali. Alisisitiza kuwa, sifa kuu ya ufundishaji wa kiugunduzi ni kumhusisha mwanafunzi na kumpa kipaumbele katika hatua zote za ufundishaji na ujifunzaji. Matumizi ya mtaala mpya huweza kutekeleza jambo hili. Huo ndio msingi uliochangia katika uteuzi wa nadharia hii kutafitia athari za mtaala mpya katika ufundishaji wa wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili zitakazochaguliwa jijini kusini mwa Mbarara.

## MSINGI WA KIDHANA

| **Kibadilika huru** | | **KibadilikaTegemezi** |
|---|---|---|
| **MTAALA MPYA** | | **UTENDAJI WA WANAFUNZI WA KISWAHILI** |
| Matumizi ya vifaa vya kisasa kama tarakilishi na simu za mkononi ili wafanye utafiti wa kutosha.<br><br>Wanafunzi kujifunza kile wanacho kiona na kukijua papo hapo.<br><br>Wanafunzi hujifunza jinsi ya kuwa wanafunzi bora, na kuwajibika kwa elimu yao. | → | Unasaidia wanafunzi kukuza ukakamavu miongoi mwao.<br><br>Mtaala mpya unasaidia wanafunzi wa Kiswahili kukuza stadi ya kusoma.<br><br>Mtaala mpya unasaidia wanafunzi wa Kiswahili kuwa na ustawi pamoja na umilisi wa lugha. |

Kulingana na kiunzi hiki, kuna kibadilika huru na kibadilika tegemezi. Kibadilika huru ni Mtaala mpya na kibadilika tegemezi ni utendaji wa wanafunzi wa Kiswahili. Kwa kuzingatia kiunzi hiki, inabainika wazi kuwa kibadilika huru kinaweza kuathiri kibadilika tegemezi kwa kukistawisha au kwa kukibana. Vipengele mbalimbali katika kiunzi hiki vinaonyesha kuwa, mtaala mpya unaweza kustawisha au kubana utendaji wa wanafunzi wa Kiswahili. Kulingana na kiunzi hiki, matumizi ya vifaa vya kisasa kama tarakilishi unasaidia wanafunzi wa Kiswahili kukuza ukakamavu miongoni mwao kwa sababu wanapofanya utafiti kuhusu jambo Fulani.

## UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA.

Kothari (2008), anaeleza kuwa uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zitakazokusanywa kwa namna ambayo zitasaidia kujibu maswali ya utafiti husika.

Data zilizokusanywa zilitolewa maelezo, zikachambuliwa na kufupishwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na wa kiidadi. Kothari (1990), anaeleza kuwa mkabala usio wa kiidadi ni njia ya kuchambua data katika muundo wa maelezo pasipo kufuata taratibu za kitakwimu.

Katika utafiti huu mkabala huu ulimwezesha mtafiti kuchambua data zilizokuwa katika maelezo kupitia njia ya mahojiano, majadiliano na kwa kutumia hojaji zilizoandaliwa na mtafiti. Aidha, Majedwali yalitumika na hivyo data hizo zilifupishwa kwa namna ambayo ni rahisi kuchambuliwa na kueleweka kwa kuzingatia malengo ya utafiti huu.

Data zilikusanywa kutoka vyanzo kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Mtafiti kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na wa kiidadi alichambua data hizo.

## UWASILISHAJI, UCHANGANUZI NA UFASIRI WA DATA

### UTANGULIZI

Sura hii inawakilisha matokeo ya utafiti juu ya uchanganuzi wa athari za mtaala mpya katika ufundishaji wa wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili zilizochaguliwa jijini kusini mwa Mbarara

Utafiti ulifanyiwa katika shule tatu zifuatazo; shule ya upili ya Heritage International, Allied High School na Shule ya upili ya Mbarara. Vilevile matokeo ya shule yaliwakilishwa kwa majedwali na Tarakwimu kisha yalichunguzwa yakafasiliwa na kuwasilishwa kwa idadi na katika kiwango cha asilimia kwa kufuatia maswali ya utafiti.

### DATA ZA WATAFITIWA/KIZIO

Watafiti walichunguza na kuchanganua data za watafitiwa kulingana na kiwango cha jinsia na umri katika shule za upili. Kwa hivyo, watafiti walichunguza vigezo hivi ili kutosheleza matokeo ya uwanjani.


**Data kutokana na malengo ya utafiti.**

### KUCHUNGUZA UMUHIMU WA MTAALA PYA KATIKA UFUNDISHAJI WA WANAFUNZI WA KISWAHILI

Watafiti walinuia kuchunguza ikiwa mtaala mpya una umuhimu wowote katika ufundishaji n utendaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za upili, watafitiwa wengi yaani 72(80%) walijibu na kusema kwamba mtaala mpya una umuhimu mkubwa katika ufundishaji na utendeji wa Kiswahili katika shule za upili na wahojiwa 18(20%)

walisema kwamba mtaala mpya hauna umuhimu wowote katika ufundishaji wa wanafunzi wa Kiswahili.

**Jedwali hili linaloonyesha maoni ya wahojiwa kuhusu umuhimu wa mtaala mpya wa Kiswahili katika shule za upili.**




**Asilia: Data za msingi 2023**

Kulingana na ugunduzi wa utafiti, watafiti waligunduwa kwamba mtaala mpya uko na umuhimu mkumbwa sana katika utendaji wa Kiswahili katika shule za upili kwa sababu asilimia kubwa ya wahojiwa 80% walisema kwamba mtaala mpya una umuhimu mkubwa sana katika ufundishaji wa Kiswahil lakini asilimia ndogo 20% ya wahojiwa walisema kwamba mtaala mpya hauna umuhimu wowote katika ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili.

Watafiti walihitimisha kwamba mtaala mpya una umuhimu mkubwa katika ufundishaji kitaaluma kwa wanafunzi wa Kiswahili katika shule za upili.

**Jewali 4 linaloonyesha Umuhimu wa mtaala mpya katika ufundishaji kitaaluma kwa wanafunzi wa Kiswahili.**

| Umuhimu wa mtaala mpya | Maoni | Marudio | Asilimia |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kutoa Maarifa Bora ya Lugha | Ndiyo | 76 | 84 |
| | Hapana | 14 | 16 |
| | **Ujumla** | **90** | **100** |
| Mtaala mpya unasaidia wanafunzi kukuza ukakamavu miongoi mwa wanafunzi kwa sababu baada ya kusoma vitabu watakuwa wanajadiliana kuhusu vitabu na katika shughuli hiyo wanaanza kujiamini wenyewe jambo linalohitajika ili kupita mitihani. | Ndiyo | 90 | 100 |
| | Hapana | 0 | 0 |
| | **Ujumla** | **90** | **100** |
| Mtaala mpya unasaidia wanafunzi wa Kiswahili kupata msamiati unaotosha ili kuongea lugha ya Kiswahili. Pia msamiati huu unawasaidia kuelewa kwa urahisi maswali wanayoulizwa katika | Ndiyo | 65 | 72 |
| | Hapana | 25 | 28 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| mitihani pamoja na kuwa na msamiati unaotosha kueleza fununu zao kwa wazi. Jambo hili linawasaidia kupita mitihani. | **Ujumla** | **90** | **100** |
| Mtaala mpya unasaidia wanafunzi wa Kiswahili kukuza ujasiri. Kwa kuwa tungo za fasihi zinawafundisha namna watu wanavyopambana na changamoto zinazo wakabili. | Ndiyo | 59 | 66 |
| | Hapana | 31 | 34 |
| | **Ujumla** | **90** | **100** |
| Wanafunzi kupata burudani kwa sababu katika mtaala huu kuna vipindi vinavyofundisha kuhusu burudani kama serehe, ndoa, sehemu za mwili nakadhalika. | Ndiyo | 70 | 78 |
| | Hapana | 10 | 22 |
| | **Ujumla** | **90** | **100** |
| Mtaala mpya unasaidia wanafunzi wa Kiswahili kuwa na ustawi pamoja na | Ndiyo | 74 | 82 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| umilisi wa lugha katika mazungumzo kwa kuwa wanapata tajriba ya uakifishaji yaani namna ya kutumia vituo vya alama kama alama ya mshangao. | Hapana | 16 | 18 |
| | **Ujumla** | **90** | **100** |

**Asilia: Data za msingi 2023**

Kulingana na matokeo ya utafiti, wahojiwa 76(84%) walisema kwamba mtaala mpya wa Kiswahili unaweza kuzingatia mbinu za kisasa za ufundishaji wa lugha, kusaidia wanafunzi kupata maarifa bora ya lugha ya Kiswahili. Hii ni muhimu kwa kuimarisha ustadi wa kusoma, kuandika, kusikiliza, na kuzungumza, wahojiwa 62(72%) walisema kwamba Mtaala mpya wa Kiswahili unasaidia wanafunzi kukuza ukakamavu miongoi mwa wanafunzi wa sababu baada ya kusoma vitabu watakuwa wanajadiliana kuhusu vitabu na katika shughuli hiyo wanaanza kujiamini wenyewe jambo linalohitajika ili kupita mitihani. Kwa mujibu wa Tyler (1949), malengo ya mtalaa ni kauli ambazo hufafanua mabadiliko ya kitabia yanayotarajiwa kutokea miongoni mwa wanafunzi baada ya kupokea mafunzo. Malengo ni muhimu kwa mwalimu anapotekeleza mtalaa kwa kuwa humwezesha kubaini stadi na maarifa mahususi ambayo mwanafunzi hutarajiwa kupata kutokana na mafunzo anayopokea (Brown,1995). Malengo haya ndiyo huelekeza shughuli ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kuwa ni kupitia kwa shughuli ya ufundishaji ndipo yanafikiwa. Utafiti ulikusudia kutambua namna malengo ya ufundishaji katika vyuo vikuu yalifikiwa. Kufikiwa kwayo kulithibitishwa kupitia kwa utendaji wa walimu wa shule za upili walipotekeleza mtalaa wa TUMIKE katika shule za upili. Tyler (1949) alibaini kuwa malengo ya mtalaa yalibuniwa kutokana na mahitaji ya wanafunzi, jamii na wataalamu. Utafiti ulikusudia kutambua namna ambavyo hali hii ilidhihirika katika malengo ya mitalaa vyuoni na shuleni.

Pia kiligunduliwa kutoka kwa wahojiwa 90(100%) ambao walisema kwamba mtaala mpya unasaidia wanafunzi kukuza ukakamavu miongoi mwa wanafunzi wa fasihi kwa sababu baada ya kusoma vitabu wanajadiliana kuhusu vitabu na katika shughuli hiyo wanaanza kujiamini wenyewe jambo linalohitajika ili kupita mitihani, wahojiwa 65(75%) walisema kwamba Mtaala mpya unasaidia wanafunzi wa Kiswahili kupata msamiati unaotosha ili kuongea lugha ya Kiswahili. Pia msamiati huu unawasaidia kuelewa kwa urahisi maswali wanayoulizwa katika mitihani pamoja na kuwa na msamiati unaotosha kueleza fununu zao kwa wazi. Jambo hili linawasaidia kupita mitihani yao, wahojiwa 59(66%) walisema kwamba mtaala mpya unasaidia wanafunzi wa kiswahili kukuza ujasiri. wahojiwa 74(82%) walisema kwamba Mtaala mpya wa Kiswahili unasaidia wanafunzi wa fasihi ya Kiswahili kuwa na ustawi pamoja na umilisi wa lugha katika mazungumzo kwa kuwa wanapata tajriba ya uakifishaji yaani namna ya kutumia vituo vya alama kama alama ya mshangao.

## SABABU ZA WALE AMBAO HAWAKUBALI KWAMBA MTAALA MPYA WA KISWAHILI INA UMUHIMU KATIKA SHULE ZA UPILI.

Walidai kwamba:

Hakuna vitabu vinavyotosha ili kuwezesha wanafunzi kutenda vizuri kitaaluma.

Hakuna muda unaotosha ili kusoma vitabu vyote ambavyo vimewekwa kwenye mtaala mpya. Wanafunzi wanasoma sehemu na kumaliza muda bila kuongezea hapo. Jambo linalowaletea kutounganisha visa na mwishowe hawahitimu katika masomo yao.

Ni kuharibu malighafi kama kununua vitabu vya kiada, warsha za walimu kuhusu majadiliano ya mtaala mpya kumbe shule na wazazi hawana fedha toshi za kugharamia mradi huo.

Pia waliendelea na kusema kwamba si kila mwanafunzi wa Kiswahili ana uwezo wa kusoma na kuielewa moja kwa moja ili kufaulu mitihani.

## KUCHUGUZA CHANGAMOTO ZINAZOJITOKEZA KATIKA UENDELEZAJI WA MTAALA MPYA WA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA UPILI.

Watafiti waliendelea na kuchunguza changamoto zinazojitokeza katika uendelezaji wa mtaala mpya wa Kiswahili katika shule za upili na matokeo ya utafiti yameonyweshwa katika jedwali hapo chini.

Kulingana na ugunduzi wa utafiti, wahojiwa wengi 32(30%) ambao walisema kwamba walimu amba ndio waendelezaji wa mtaala mpya hii ya Kiswahili hawakupewa elimu ya ziada ili kupambana na mtaala mpya. Tafiti mbali mbali zinaonesha kwamba mchakato wa kuwaandaa walimu wa shule za upili unakumbwa na changamoto nyingi kote ulimwenguni. Goodlad (1995,1984) anasema kuwa maandishi mengi kuhusu taaluma ya elimu yameibua mijadala kuhusu changamoto zinazodhihirika katika maandalizi ya walimu wa shule za upili. Baadhi ya changamoto hizo huwaathiri walimu wanapotekeleza mitalaa ya shule za upili. Utafiti uliofanywa na Miller na Silvernail (2000) unaonyesha kwamba namna walimu wa shule za upili walivyofunza baada ya kuhitimu hakuambatani na mafunzo ya ualimu waliyoyapokea katika vyuo vikuu.

Miller na Silvernail wanasema kwamba yale ambayo walimu huyafanya wanapokuwa nyanjani kutekeleza yaliyomo kwenye mitalaa ya shule za upili ni mambo ambayo wanajua yanatarajiwa kutoka kwao kama walimu na wala hawayahusishi na mafunzo ya ualimu waliyoyapata. Lynch (2003) anasema kwamba utafiti uliowahi kufanyika katika chuo kikuu kimoja kulinganisha njia za ufundishaji zilizotumika kuwaandaa walimu wakiwa chuoni na zile walizotumia nyanjani wakati wa mazoezi ya ufundishaji uligundua kwamba

kulikuwa na tatizo katika maandalizi ya walimu. Tatizo lilikuwa kwamba mada ambazo walimu walifundishwa vyuoni hazikuwafaa walipofundisha katika shule za upili. Hivyo basi, walimu walitatizika walipowasilisha mafunzo yao wakiwa nyanjani kwenye mazoezi ya kufundisha, wahojiwa 12(36%) walisema kwamba waendelezaji wa mtaala mpya hii ya ufundishaji wa kiswahili yaani walimu hawakuzingatiwa katika mchakato wa kutengeneza mtaala mpya , wahojiwa 10(11%) walieleza kwamba kuna ukosefu wa uhamasishaji wa wazazi na wanafunzi kuhusu umuhimu wa mtaala mpya wa ufundishaji wa Kiswahili kwa sababu hawa ndio waendelezaji wa mtaala mpya hii kama katika kununua vitabu mbalimbali vya riwaya, tamthilia na nadhari, wahojiwa 21(23%) walisema kwamba walimu hawapewi usaidizi unaotosha kutoka kwa walimu wakuu, wazazi na kituo kikuu cha mtalaa kama vitabu vya kiada na vitabu vya kuongoza walimu. Baadhi ya walimu wanajigharamia wenyewe kupata vitabu vya kiada, na wahojiwa 9(10%) walisema kwamba kuna ukosefu wa motisha miongoni mwa waendelezaji wa mtaala mpya.

## NAMNA YA KUTATUA CHANGAMOTO ZINAZOJITOKEZA KATIKA UENDELEZAJI WA MTAALA MPYA WA KISWAHILI.

Kulingana na matokeo ya utafiti, utafiti uligundua kwamba changamoto zinazojitokeza katika uendelezaji wa mtaala mpya wa Kiswahili zinaweza kutatuliza. Kwa sababu wahojiwa wote walikubali kwamba changamoto hizo zinaweza kutatuliwa kupitia njia zifuatazo;

Kulingana na mahojiano mtafiti aliyofanya kuhusu utatuzi wa changamoto hizo, wahojiwa kumi waliowakilisha asilimia kumi na saba walisema kwamba wazazi pia wachangie katika kuendeleza mtaala mpya kwa kununua vitabu ambavyo vipo kwenye mtaala mpya. Kwa mfano wazazi wakinunulia watoto wao vitabu, wanafunzi hawa watakuwa na muda unaotosha kuvisoma kwa sababu watakuwa wanavimiliki kila mara.

Wahojiwa tisa waliowakilisha asilimia kumi na tano walisema kwamba viongozi wa shule wajaribu huku na kule kuona kwamba wamenunua vitabu vya kiada na vifaa vingine kama filamu za tamthilia kulingana na mabadiliko ya mtaala mpya. Jambo hili huwezesha walimu kufundisha bora wanafunzi na mwishoni wanazuka na utendaji bora kitaaluma.

Wahojiwa tano waliowakilisa asilimia nane walisema kwamba ili kutatua changamoto zinazojitokeza katika uendelezaji wa sera ya ufundishaji wa lugha ya Kiswahili, Wizara ya elimu iangalie kwamba walimu wamepewa elimu ya ziada kuhusu mabadiliko ya mtaala mpya ili kupata ujuzi na stadi za kufundisha vyema. Walimu wakifundishwa tena wanapata stadi na hamu ya kwendeleza mtaala mpya, jambo linaloletea wanafunzi kufaulu mitihani kwa sababu watakuwa wanaielewa vyema kutokana na walimu. Maoni ya wahojiwa haya yanaoana na ya MacArthur na Baron (1983) ambao wanasema kuwa mwalimu aliyeandaliwa vyema anaweza kutegemewa katika kuutekeleza mtalaa. Kwa mujibu wa Oyedeji (1998), lengo kuu la kuutekeleza mtalaa ni kuhakikisha kuwa ujifunzaji umetokea miongoni mwa wanafunzi. Hili huweza kufikiwa iwapo kutabuniwa mbinu bora za kufundisha katika viwango vyote vya elimu (Makoti, 2017). Simala (2019) anaeleza kuhusu umuhimu wa kuwapa walimu mafunzo bora ikiwa watategemewa katika kutekeleza mitalaa ipasavyo. Anasema kuwa taratibu zinazozingatiwa na walimu katika utekelezaji wa mitalaa huhitaji mafunzo ya hali ya juu. Kwa hivyo, walimu walioandaliwa vyema wanao ujuzi wa kutekeleza mtalaa uliopo ili kuwapa wanafunzi ujuzi wa kukabiliana na hali mbalimbali za maisha.

Kama tunavyojua kwamba walimu ni kundi moja miongoni mwa waendelezaji wa mtaala mpya. Lazima wapewe nafasi ya kuchangia katika mfumo wa kutengeneza mtaala mpya. Hii ni njia moja inayowapendeza kuendeleza mtaala mpya kama kitu chao na mwishowe wanafunzi wanafaidika kwa kupata wanachotarajia na kufaulu mitihani. Jambo hili lilitolewa na wahojiwa kumi na wawili ambaowaliwakilisha asilimia ishirini waliohojiwa.

Kulingana na wahojiwa saba waliowakilisha asilimia kumi na mbili, walisema kwamba Kituo kikuu cha mtalaa kinapaswa kuanza na

kuhamasisha walimu, wazazi na wanafunzi kuhusu umuhimu wa mabadiliko ya mtaala mpya. Hiki kinawapatia motisha ya kukaribisha na kuendeleza mtaala mpya bila shaka jambo ambalo linasababisha wanafunzi kufanikiwa katika somo.

Pia wahojiwa kumi waliowakilisha asilimia kumi na saba walisema kwamba kituo kikuu cha mtalaa (NCDC) kinapaswa kupatia shule vifaa vya kufundishia kama vitabu vya kiada ili kulazimisha kazi ya uendelezaji wa mtaala mpya. Pakiwepo vitabu vinavyotosha mwalimu anaweza kuwaongoza wanafunzi basi wakawa na uwezo wa kusoma kwao wenyewe bila mwalimu ikiwa amepata shida na siku hiyo hayupo na mwishoni wanafaulu mitihani.

Na wahojiwa saba waliowakilisha asilimia kumi na mbili walisema kwamba walimu na wanafunzi wanapaswa kugawana maarifa kupitia kubadilishana mawazo kuhusu mtaala mpya ili kutatua shida ya uchache wa vitabu vya kiada. Hiki kinawezakana kwa kutumia mijadala ya ndani ya shule na nje kuhusu vitabu vya kiada vipya yaani vya fasihi. Pia na kukopeshana vitabu vya kiada.

**Muktasari wa matokeo ya msingi.**

Utafiti ulifanyika ili kuchunguza uhusiano uliopo baina ya mtaala mpya wa ufundishaji wa Kiswahili na utendaji kitaaluma kwa wanafunzi wa Kiswahili.

Kwa ujumla watafitiwa tisini kutoka shule za upili tatu walishiriki katika utafiti huu ambao ni walimu na wanafunzi wa Kiswahili katika shule za upili.

Data za watafitiwa zilizozingatiwa katika utafiti ni jinsia na umri. Kwa kiwango cha jinsia wanaume walikuwa wanazidi wanawake yaani thelathini waliowakilisha asilimia hamsini.

Pia katika kiwango cha umri watafitiwa wengi walikuwa katika kundi la miaka kati ya kumi na tano na ishirini yaani washiriki thelathini na tisa waliowakilisha asilimia tisini na tano Pia kulikuwepo na ule wa miaka arubaini na zaidi na alikuwa mwalimu.

## UMUHIMU WA MTAALA MPYA WA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA UPILI

Kilikubaliwa kwamba mtaala mpya una umuhimu kwa kuwa washiriki tisini na wawili waliowakilisha asilimia tamanini na saba walikubali na washiriki kumi na nane tu ndio walisema kwamba mtaaala mpya wa ufundishaji wa kiswahili hauna umuhimu wowote na wanaendelea na kutoa sababu kwamba vitabu vya kiada havitoshi.

Waaminifu wa mtaala mpya wa ufundishaji wa Kiswahili waliendelea na kutoa sababu kwamba mtaala mpya wa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za upili unasaidia wanafunzi zaidi sana wa fasihi ya kiswahili kukuza stadi za lugha kama kusoma, kuandika, kuongea na kusikiliza, kukuza ukakamavu, kukuza umoja, kupata msamiati.

## CHANGAMOTO ZINAZOJITOKEZA KATIKA UENDELEZAJI WA MTAALA MPYA WA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA UPILI.

Watafitiwa wote walikubali kwamba mtaala mpya wa ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili unazusha changamoto yaani watafitiwa tamanini wanaowakilisha mia moja wahojiwa walitoa changamoto kama, waendelezaji wa sera yaani walimu hawakuzingatiwa katika mchakato wa kutengeneza mtaala mpya, ukosefu wa motisha miongoni mwa waendelezaji wa mtaala mpya, walimu hawapewi usaidizi unaotosha, walimu hawapewi elimu ya ziada kuhusu mabadiliko ya mtaala mpya na hakuna vitabu vya kiada vinavyotosha.

Kuhusu mtaala mpya wa Kiswahili walisema kwamba kuna athari mbaya kwa utendaji kitaaluma kama kutozingatia walimu katika utengenezaji wa mtaala mpya jambo linalosababisha ukosefu wa motisha ya kuiendeleza mtaala mpya, walimu kutopewa elimu ya ziada kuhusu mabadiliko ya mtaala mpya. Jambo hili linasababisha walimu

kukosa umilisi na tajriba ya kuendeleza mtaala mpya ilivyo, walimu na wanafunzi hawapewi usaidizi kama vitabu vya kiada vinavyofaa. Jambo hili linatatiza uendelezaji wa mtaala mpya kwa hatua zinazotarajiwa, changamoto ya uvivu wa kusoma kwa baadhi ya walimu na wanafunzi na mtaala mpya hii mpya inahitaji kusoma kwahivyo uendelezaji wa mtaala mpya unashikwa nyuma, pia ukosefu wa kuhamasisha kunasababisha ukosefu  wa hamu katika somo moingoni mwa wanafunzi, walimu, wazazi na walimu wakuu.

## NAMNA YA KUTATUA CHANGAMOTO ZINAZOJITOKEZA KATIKA UENDELEZAJI WA MTAALA MPYA WA KISWAHILI.

Watafitiwa wote tisini waliowakilisha asilimia mia moja walikubali kwamba changamoto zinazosababishwa na sera ya ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili zinaweza kutatuliwa.

Waliendelea na kufasiri kwamba changamoto zinazozushwa na mtaala mpya wa kiswahili zinaweza kutatuliwa kama ifuatayo,

Wizara ya elimu iangalie kwamba walimu wamefundishwa tena kuhusu mtaala mpya ili kupata ujuzi na stadi za kufundisha vyema. Walimu wakipewa elimu ya ziada wanapata stadi na hamu ya kwendeleza mtaala mpya jambo linaloletea wanafunzi kufaulu mitihani kwa sababu watakuwa wanaielewa vyema kutokana na maelezo ya walimu wenye ujuzi.

Pengine waliendelea na kusema kwamba viongozi wa shule wajaribu huku na kule kuona kwamba wamenunua vitabu vya kiada na vifaa vingine kama filamu za tamthilia kulingana na mtaala mpya. Jambo hili huwezesha walimu kufundisha bora wanafunzi na mwishoni wanazuka na utendaji bora kitaaluma.

Wazazi pia wachangie katika kwendeleza mtaala mpya kwa kununua vitabu ambavyo vipo kwenye mtaala mpya waani vitabu vya

kiada. Kwa mfano wazazi wakinunulia watoto wao vitabu hivi, wanafunzi hawa watakuwa na muda unaotosha kuvisoma kwa sababu watakuwa wanavimiliki kila mara kinachowapatia muda unaotosha kuvisoma.

Kama tunavyojua kwamba walimu ni kundi moja miongoni mwa waendelezaji wa mtaala mpya. lazima wapewe nafasi ya kuchangia katika mfumo wa kutengeneza mtaala mpya. Hii ni njia moja inayowapendeza kuendeleza mtaala mpya kama kitu chao na mwishowe wanafunzi wanafaidika kwa kupata wanachotarajia na kufaulu mitihani.

Kituo kikuu cha mtalaa kinapaswa kuanza na kuhamasisha walimu, wazazi na wanafunzi kuhusu umuhimu wa mabadiliko ya mtaala mpya. Hiki kitawapatia motisha ya kukaribisha na kuendeleza mtaala mpya bila shaka jambo ambalo linasababisha wanafunzi kufanikiwa katika somo.

Walimu na wanafunzi wanapaswa kugawana maarifa kupitia kubadilishana mawazo kuhusu mtaala mpya ili kutatua shida ya uchache wa vitabu vya kiada. Hiki kinawezakana kwa kutumia mijadala ya ndani ya shule na nje kuhusu vitabu vya kiada vipya yaani vya fasihi. Pia na kukopeshana vitabu vya kiada.

## Hitimisho

Kulingana na matokeo ya uwanjani mtaala mpya wa Kiswahili unahusiana sana na utendaji kitaaluma kwa wanafunzi wa Kiswahili lakini ili kuiendeleza mtaala mpya ipasavyo ni jukumu la walimu wakuu, walimu, wazazi, wanafunzi, serikali pamoja na kituo kikuu cha mtalaa ni lazima kujiunga pamoja kwa lengo moja.

## MAPENDEKEZO

Kulingana na matokeo ya uwanjani yanathibitisha kwamba masuala yafuatayo yachukuliwe kwa makini ili kuendeleza mtaala mpya wa Kiswahili.

Utafiti huu ulipendekeza kuwa pafanyike mabadiliko ya mara kwa mara ya mitalaa hasa katika shule za upili kwa kuwahusisha walimu pamoja na waandalizi wa walimu ili wakadirie malengo, mada, mbinu za utekelezaji na tathmini mintarafu maandalizi yanayotolewa kwa walimu. Hali hii itawezesha walimu kutoa mchango wao kuhusu changamoto za mtalaa wanaotekeleza na mabadiliko wanayotarajia yafanyike. Kuhusika kwa waandalizi wa walimu kutawawezesha kutoa mafunzo kwa kuzingatia mabadiliko hayo. Kwa kufanya hivi watawaandaa walimu kuukabili mtalaa vilivyo.

Kuendeleza mtaala mpya ni jukumu la wote yaani walimu, walimu wakuu, wazazi, serikali pamoja na kituo kikuu cha mtalaa. Kwa hivyo kila mtu ajitahidi kutimiza jukumu lake ipasavyo.

Pengine walimu wapewe elimu ya ziada kuhusu mtaala mpya ili kupata stadi za kuiendeleza mtaala mpya kama inavyotarajiwa.

Wizara ya elimu iangalie kwamba walimu wamepewa elimu ya ziada kuhusu mabadiliko ya mtaala mpya ili kupata ujuzi na stadi za kufundisha vyema. Walimu wakipewa elimu ya ziada wanapata stadi na hamu ya kwendeleza mtaala mpya jambo linaloletea wanafunzi kufaulu mitihani kwa sababu watakuwa wanapata mwongozo mzuri kutoka walimu.

Pengine lazima viongozi wa shule wajaribu huku na kule kuona kwamba wamenunua vitabu vya kiada na vifaa vingine kama miongozo ya walimu inayofasili vitabu vya kiada. Jambo hili huwezesha walimu kufundisha bora wanafunzi na mwishoni wanazuka na utendaji bora kitaaluma.

Wazazi pia wachangie katika kwendeleza mtaala mpya kwa kununua vitabu ambavyo vipo kwenye mtaala mpya. Kwa mfano wazazi wakinunulia watoto wao vitabu hivi, wanafunzi hawa watakuwa na muda unaotosha kuvisoma kwa sababu watakuwa wanavimiliki kila mara.

Walimu ni kundi moja miongoni mwa waendelezaji wa mtaala mpya. Lazima wapewe nafasi ya kuchangia katika mfumo wa

kutengeneza mtaala mpya. Hii itakuwa njia moja inayowapendeza kuendeleza mtaala mpya kwa upendo wa dhati kama kitu chao na mwishowe wanafunzi wanafaidika kwa kupata wanachotarajia na kufaulu mitihani.

Kituo kikuu cha mtalaa kinapaswa kuanza na kuhamasisha walimu, wazazi na wanafunzi kuhusu umuhimu wa mabadiliko ya mtaala mpya. Hiki kinawapatia motisha ya kukaribisha na kuendeleza mtaala mpya bila shaka jambo ambalo linasababisha wanafunzi kufanikiwa katika somo.

## MAREJELEO

Allright, R. L. (1981). What do we want teaching materials for? ELT Journal, 36 (1), 5-18.

Babusa, H. (2010). Uchanganuzi Linganuzi wa Mielekeo na Umilisi wa Lugha ya Kiswahili wa Wanafunzi Katika Mikoa ya Pwani na Nairobi Nchini Kenya.

Besha, R. M. (1994). Utangulizi wa lugha na isimu. Dar-res-Salaam: Dar-es-Salaam University Press:

Brown, H. D. (2007). Principles of Language Learning and Teaching (5th Ed.). New York: Pearson Education White Plains

Buliba na wenzake (mwaka haujulikani). Misingi ya Nadharia na mbinu za utafiti. Mwanza: Serengeti Educational publishers.

Celce-Murcia, M. (1991). Grammar Pedagogy in Second and Foreign Language Teaching. New York: Newburry House.

Cohen, L. (1980). Research methods in Education (5th edition). London: Rutledge. Falmer.

Enon, C. J. (1995). Educational Research, Statistics and Measurement. Kampala: Makerere University Press.

Haki Elimu, (2011). Je walimu wetu wana sifa za ualimu na hamasa ya kufundisha? Dar-es- Salaam: Haki Elimu.